ISSN 2820-2686 | Toleo Maalumu | 2023

JARIDA MAALUMU LA

# MIAKA MITANO YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI







**Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## MAADHIMISHO YA MIAKA MITANO YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

05 Juni, 2023

JKCC - Dodoma

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. 04 | UTANGULIZI |
| UK. 07 | KUTOKA MEZANI KWA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA |
| UK. 09 | KUTOKA MEZANI KWA WAKILI MKUU WA SERIKALI |
| UK. 11 | KUTOKA MEZANI KWA NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI |
| UK. 16 | KUTOKA KWA WAKILI MKUU WA SERIKALI WA KWANZA |
| UK. 17 | KUTOKA KWA NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI WA KWANZA |
| UK. 19 | TULIPOTOKA: UZINDUZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI |
| UK. 31 | TULIPO SASA: UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI NA MAFANIKIO KUANZIA JULAI 2018- MACHI 2023 |
| UK. 42 | MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO PAMOJA NA MATARAJIO |

# VIONGOZI WA MIAKA 5 YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI



**DKT. JULIUS C. MASHAMBA**
Wakili Mkuu wa Serikali
Aprili, 2018 - Julai, 2020



**GABRIEL P. MALATA**
Wakili Mkuu wa Serikali
Julai, 2020 - Agosti, 2022

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali
Septemba, 2019 - Julai, 2020



**DKT. BONIPHACE N. LUHENDE**
Wakili Mkuu wa Serikali
Tokea Oktoba, 2022

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali
Julai, 2020 - Oktoba, 2022





**DKT. ALLY S. POSSI**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali
Apr, 2018 - Sep, 2019



**SARAH D. MWAIPOPO**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali
Tokea Oktoba, 2022



Jengo lililotumiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mara kwanza kama linavyoonekana pichani

# Utangulizi

Kwa historia, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwepo mara baada ya kupata uhuru hadi mwaka 1966 ambapo majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yalihamishiwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Sheria Na. 11 ya mwaka 1966 iliyosainiwa tarehe 6 Januari 1966.

Hata hivyo, mwaka 2018 yalifanyika marekebisho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 48 la Mwaka 2018, [*(Office of the Attorney - General (Re-structure) Order, 2018. (GN.No. 48 of 2018)*], na kuanzishwa kwa Ofisi tatu ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Madhumuni ya mabadiliko haya ilikuwa ni kuboresha sekta ya Sheria. Kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kulikusudiwa katika kuiwezesha Serikali kuwakilishwa vyema Mahakamani na katika Mabaraza ya Usuluhishi

ndani na nje ya nchi.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa kwa Hati Idhini (Instrument) ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018 *[The Office of the Solicitor General (Establishment Order) 2018]*. Hati idhini hiyo ilitolewa kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, tarehe 13 Februari, 2018. Uanzishwaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu ulienda sambamba na uteuzi wa Wakili Mkuu wa Serikali na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 15 Aprili, 2018. Katika uteuzi huo, Dkt. Julius Clement Mashamba aliteuliwa kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Dkt. Ally Saleh Possi kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali.

Miaka mitano imepita tokea kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Malengo ya kuanzishwa kwa Ofisi hii ni kuwezesha Serikali kuwa na mfumo madhubuti wa usimamizi wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi kitaifa na kimataifa. Baada ya miaka mitano, wadau wanayo haki ya kufahamu iwapo matarajio ya Serikali kufuatia kuanzishwa kwa Ofisi hii yamefikiwa.

Jarida hili Maalumu limeandaliwa kwa lengo la kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa miaka mitano tangu kuanzishwa kwake likiwa na Kaulimbiu isemayo "**Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali: Tulipotoka, Tulipo na Tunapoelekea**".

Katika kutimiza adhima hii, Jarida hili linaelezea historia ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Malengo, Dhima, Dira na Mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwake. Pia, linaangazia changamoto zinazohusiana na utekelezaji wa majukumu na mikakati iliyochukuliwa ili kukabiliana na changamoto hizo.

Kupitia Jarida hili Maalumu, wadau wetu wataweza kufahamu kwa kina shughuli mbalimbali zilizofanywa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake na mwelekeo wa Ofisi kwa vipindi vinavyokuja kutokea sasa.

Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inawashukuru sana wadau wetu wote muhimu ndani na nje ya Serikali kwa kuendelea kutuamini na kutoa ushirikiano uliowezesha kutekelezwa vyema kwa majukumu ya Ofisi hii muhimu.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 11 OF 1966

I ASSENT,

Julius K. Nyerere

President

6TH JANUARY, 1966

**An Act to make provision for the Transfer of the Duties, Powers and Functions of the Solicitor-General**

[1ST OCTOBER, 1965]

ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

*Short title and commencement*

1. This Act may be cited as the Solicitor-General (Transfer of Duties and Powers) Act, 1965 and shall be deemed to have come into operation on the first day of October, 1965.

*Duties and functions of the Solicitor-General may be exercised or performed by the Attorney-General or his representative*

2.—(1) Subject to this section, where by or under any written law any duty is imposed or any power or function is conferred on the Solicitor-General, such duty may be performed and such power or function may be exercised by the Attorney-General or such legally qualified person holding office in the Attorney-General's Chambers as the Attorney-General may in writing nominate in that behalf.

(2) Where by or under any written law the Solicitor-General is appointed a member of any board, commission or committee—

(a) together with the Attorney-General, the Attorney-General may, by notice in writing addressed to such board, commission or committee, nominate any legally qualified person holding office in the Attorney-General's Chambers to be such member in place of the Solicitor-General, and upon such nomination such person shall be deemed to have been appointed such member in place of the Solicitor-General;

(b) in any other case, the Attorney-General may, by notice in writing addressed to such board, commission or committee, nominate either himself or any legally qualified person holding office in the Attorney-General's Chambers to be such member in place of the Solicitor-General, and upon such nomination the Attorney-General or such person, as the case may be, shall be deemed to have been appointed such member in place of the Solicitor-General.

**Sheria iliyohamisha majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

# KUTOKA MEZANI KWA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA



**Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.)**

**Waziri wa Katiba na Sheria**

Tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, yapo mambo mengi makubwa ambayo yametekelezwa kwa ufanisi na Ofisi hii. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kuisaidia Serikali katika kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Serikali kupitia Ofisi hii, imeweza kutumia Mawakili wake katika kuendesha Mashauri yote kwenye mabaraza ya Kimataifa, ikiwemo Baraza la Kimataifa la Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (**International Centre for Settlement of Investment Disputes -ICSID**); Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya London (**London Court of International Arbitration**) Mahakama ya kudumu ya Usuluhishi (**The Permanent Court of Arbitration- PCA**) na Kituo cha Kimataifa cha Biashara (**International Chamber of Commerce - ICC**).

Kwa uwezeshaji wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa sasa inasimamia mashauri yote ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi isipokuwa kama itaonekana

kuwepo kwa ulazima wa kuhusisha mawakili binafsi hususani pale inapotokea shauri husika lipo katika nchi ambayo Sheria zake haziruhusu Uwakilishi kutoka kwa Mawakili ambao hawajasajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi husika.

Kuwepo kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, kumesaidia kupunguza gharama zilizokuwa zinalipwa kwa Mawakili binafsi ambapo kwa tathmini iliyofanyika hivi karibuni, gharama za kulipa Mawakili binafsi wa nje ya nchi kwa shauri moja ilikuwa haipungui kiasi cha shilingi Bilioni 5 kabla ya kuanzishwa kwa Ofisi hii.

Kufuatia kuanzishwa kwa Ofisi hii gharama ya uendeshaji wa shauri moja la kimataifa imepungua na kufika kati ya shilingi milioni 500 mpaka Bilioni 1 ambazo kwa ujumla zimekuwa zikitumika kugharamia Mashauri ikiwemo kuandaa mashahidi, nyaraka pamoja na gharama za kusafiri iwapo Mashauri yatasikilizwa nje ya nchi.

Katika kipindi cha miaka mitano tokea kuanzishwa kwake, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuokoa fedha nyingi za Serikali kutokana na kushinda Mashauri.

Aidha, kutokana na kutumia Mawakili wa Serikali kuendesha Mashauri ya kimataifa, Serikali imeweza kuwajengea uwezo kitaaluma Mawakili wake hatua iliyopelekea umakini na weledi wa hali ya juu katika usimamizi na uendeshaji wa Mashauri na kuzuia uvujaji wa siri za Serikali.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeweza kusaidia Serikali kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa migogoro inayosababisha Mashauri na kuwa na takwimu sahihi za Mashauri yanayohusu Serikali kupitia kanzi data iliyoanzishwa.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuiwakilisha vyema Serikali katika mashauri mbalimbali ya Madai na Usuluhishi ndani na nje ya nchi. Pia tumeshuhudia idadi ya kutosha ya Mawakili wa Serikali wakipatiwa hati idhini ya kuendesha Mashauri ya Serikali Mahakamani; sambamba na kuwajengea uwezo Mawakili kupitia mafunzo mbalimbali ya kitaaluma kwa lengo la kuongeza ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya ndani na nje ya nchi.

Kwa kutambua umuhimu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kutoa ushirikiano kwa Ofisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Kwa moyo wa dhati, napenda kuishukuru Serikali chini ya Uongozi thabiti wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiamini na kuiongezea bajeti Ofisi ya Wakili Mkuu ili kutekeleza vyema majukumu yake.

Naipongeza pia Menejimenti chini ya uongozi wa Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya. Pia, nawashukuru sana Mawakili Wakuu waliopita ambao ni Dkt. Julius Clement Mashamba na Mhe. Jaji Gabriel Pascal Malata pamoja na Naibu Wakili Mkuu aliyepita Dkt, Ally Saleh Possi kwa kuweka msingi uliosaidia Ofisi hii kuwa mahiri kwa kipindi cha miaka mitano tangu ilipoanzishwa. Nawashukuru pia Mawakili na watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kulitetea Taifa letu.

# KUTOKA MEZANI KWA WAKILI MKUU WA SERIKALI



**Dkt. Boniphace Nalija Luhende**
**Wakili Mkuu wa Serikali**

Ni furaha yangu kuleta kwenu Jarida hili Maalumu la miaka mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Uamuzi wa kuianzisha tena Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ulitokana na nia thabiti ya Serikali ya kuleta na kuongeza ufanisi zaidi katika kusimamia, kuratibu na kuendesha Mashauri za madai na usuluhishi yanayoihusu Serikali katika Mahakama na mabaraza ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Ikumbukwe kuwa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwepo hapo awali kabla ya Serikali kuamua kuhamishia majukumu yake ya kuendesha, kuratibu na kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnamo mwaka 1966.

Tokea kuanzishwa kwake, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kufanya mambo mengi kwa ufanisi mkubwa na kuisaidia Serikali kutimiza adhima ya kuanzisha Ofisi hii.

Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Wakili Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 10 Oktoba, 2022, toka kwenye nafasi niliyokuwa nayo awali ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, kufuatia uteuzi wa Mhe. Rais alioufanya tarehe 10 Julai, 2020.

Ninaahidi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii ili kupitia ofisi hii Serikali iweze kuwakilishwa vyema katika uendeshaji wa Mashauri za Serikali katika Mahakama na Mabaraza ya Usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Naishukuru menejimenti, watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na viongozi wote walionitangulia kwa ushirikiano mkubwa walionipatia ambao umekuwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Taasisi nyingine za Serikali imeweza kutekeleza majukumu yake ya kuendesha, kuratibu na kusimamamia mashauri mbalimbali ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa ufanisi mkubwa. Kupitia jukwaa hili nitaeleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa na ofisi hii kwa kuwa mengi yameelezewa humu kwa kina ndani ya jarida hili. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo;-

(i) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kukamilisha muundo wa Ofisi na kuteua Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo;

(ii) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuandaa Mpango Mkakati wa Kuboresha na kuimarisha Takwimu za uendeshaji wa mashauri yote ya Madai na Usuluhishi nchini;

(iii) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuanza ujenzi wa jengo lake Makao Makuu ya nchi Dodoma ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi Mikoani ambapo kwa sasa Ofisi imefanikiwa kufungua Ofisi katika mikoa kumi na saba (17) zenye masijala ya Mahakama Kuu.

(iv) Pia Ofisi inaendelea kujiimarisha katika maeneo mbalimbali tokea kuanzishwa kwake, ambapo ofisi hii imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya Uratibu, Usimamizi, Ushauri, na Uendeshaji wa Mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa dhidi au kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

Kwa niaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali napenda kuwahakikishia kuwa tutaendelea kufanya kazi tuliyokabidhiwa kwa weledi na uadilifu mkubwa kwa kutekeleza ipasavyo malengo ambayo kwayo ilianzishwa. Aidha, tunatambua matarajio ya Serikali na Taasisi zake kwa ofisi hii, hivyo tunaahidi kuwa tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha tunatekeleza majukumu hayo na kufikia matarajio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusimamia mashauri kwa uledi na kwa ufanisi, pamoja na kusimamia majadiliano ya mashauri nje ya mahakama hatua itakayosaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri pamoja na kukuza imani ya wananchi kwa Serikali yao kupitia uendeshaji wa mashauri ndani na nje ya nchi.

Kazi Iendelee!

# KUTOKA MEZANI KWA NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI



**Sarah D. Mwaipopo**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Mnamo tarehe 10 Oktoba 2022 niliteuliwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Nilijiunga na Ofisi hii kama Naibu Wakili Mkuu wa Serikali wa kwanza mwanamke nikitokea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwaka huu 2023, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetimiza miaka mitano tangu kuanzishwa kwake mnamo tarehe 13 Februari 2018, kupitia Gazeti la Serikali Na. 50/2018. Kuanzishwa kwa Ofisi hii kulitokana na maboresho yaliyofanywa kwenye Sekta ya Sheria na huduma za umma mnamo mwaka 2018 hususan yakihusisha marekebisho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Gazeti la Serikali Na. 48/2018. Kufuatia marekebisho hayo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa sambamba na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Aidha, baadhi ya Divisheni zilizokuwa zikiunda Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilifutwa na kuwa

sehemu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Divisheni hizo ni pamoja na Divisheni ya Mashauri ya Madai na Usuluhishi na iliyokuwa Divisheni ya Katiba na Haki za Binadamu ambayo nilikuwa nikiiongoza kama Mkurugenzi kabla ya mabadiliko hayo ya Muundo.

Kama Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ninatambua kazi na michango ambayo imefanywa na Manaibu Wakili Wakuu wa Serikali walionitangulia ambao ni Dkt. Ally Possi, kwasasa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi na Ujenzi akisimamia eneo la Uchukuzi, Mhe. Gabriel Malata Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Dkt Boniface Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali ambao wamehudumu katika Ofisi hii kwa vipindi tofauti. Aidha, ninatarajia kuendeleza kazi iliyofanywa watangulizi wangu na kuendelea kutekeleza mikakati na mipango mipya ya Ofisi kwa maslahi ya Taifa letu.

Tunapotathmini kipindi cha miaka mitano ya Ofisi hii tunatambua mchango mkubwa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha Ofisi hii inaanzishwa tena upya, inaimarishwa na inawezeshwa kupiga hatua za uboreshaji wa huduma zake kwa Serikali na Wadau wake. Kwa muktadha huo, tumeona haja ya kufanya tathmini ya wapi tulipotoka, tulipo na tunapoelekea kwa mujibu wa Dira yetu ya kuwa Taasisi Mahiri ya Umma ya Uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi. Dira hii imejengwa chini ya msingi wa Dhima ya kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai, kikatiba, haki za binadamu, uchaguzi na usuluhishi kwa niaba ya Serikali kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu.

Nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiamini Ofisi hii na kuipatia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, niwapongeze Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango Makamu wa Rais pamoja na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kumsaidia Mhe. Rais kuiletea



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na watumishi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kibaha mkoani Pwani.*

nchi yetu maendeleo, hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati nchi nzima, ikiwamo ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na Miradi mingineyo.

Nichukue fursa hii kueleza machache ambayo yameweza kurekodiwa katika kipindi hicho na Mikakati ambayo tumepanga kuitekeleza katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha;

(i) Bajeti: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilipitishiwa Bajeti ya Shilingi bilioni 4.17 mnamo mwaka 2018/2019. Bajeti hiyo iliendelea kutolewa kwa viwango vifuatavyo kwa miaka ya fedha iliyofuatia ; Shilingi bilioni 7.29 kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; Shilingi bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Katika kipindi cha awamu ya sita ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliongezewa bajeti yake kutoka Shilingi bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi Shilingi bilioni 12.13 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 5. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 ilipatiwa Shilingi billioni 12.81 na katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Ofisi imepatiwa bajeti ya Shilingi billion 17.07 sawa na ongezeko la asilimia 25 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2022/23. Kuongezeka kwa bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutaiwezesha Ofisi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya usimamizi na uendeshaji Mashauri ya Madai na Usuluhishi kwa niaba ya Serikali kwa ufanisi na kupunguza changamoto zinazotokana na ufinyu wa bajeti uliokuwepo hapo awali. Dira yangu ni kuhakikisha kuwa Bajeti ya kawaida ya Ofisi inaendelea kuongezeka kwa kuzingatia ukubwa wa majukumu iliyonayo na mahitaji halisi yaliyopo, kazi ambayo tayari imekwishaanza kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mikakati mingineyo iliyopo ni pamoja na kuhakikisha Ofisi inapata Bajeti ya Maendeleo itakayotumika sambamba na Bajeti ya Serikali. Kazi ya maandalizi ya maandiko ya kujenga hoja ya upatikanaji wa rasilimali fedha inaendelea.

(ii) Ajira na Watumishi: Wakati wa uanzishwaji wake mnamo mwaka 2018/2019, Ofisi ilianza na idadi ya watumishi 86. Hadi kufikia Mei 2023 Ofisi ilikuwa na watumishi 233 wakiwemo Mawakili wa Serikali 128. Kwa Mwaka ujao wa Fedha 2023/2023 Ofisi imepanga kuendelea kutekeleza Kibali cha kuajiri watumishi 40 kilichotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ikiwemo Mawakili 29. Sambamba na ajira mpya, Ofisi imepanga kuendelea kusimamia rasilimali watu iliyopo kwa lengo la kuhakikisha inaendelea kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yake.

(iii) Muundo na Muundo wa Kiutumishi :Kufuatia Muundo wa Ofisi uliopitishwa na Ofisi ya Rais mwaka 2018, Ofisi hii iliundwa na Divisheni nne (4) na Vitengo saba (7). Aidha, katika kipindi cha Miaka mitano Ofisi imeweza kuanzisha jumla ya Ofisi 17 katika Mikoa ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni pamoja na Dar es salaam, Tanga, Morogoro, Musoma, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya Iringa, Kigoma, Tabora, Mtwara, Songea, Dodoma, Kagera na Sumbawanga. Uanzishwaji wa Ofisi hizi umewezesha uwakilishi wa Serikali

kwenye mashauri yanayofunguliwa katika mikoa husika na usogezaji wa huduma za kisheria kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha tumepanga kuanzisha Ofisi mpya ya Manyara kufuatia kufunguliwa kwa Kanda mpya ya Mahakama Kuu Mkoani Manyara na Masjala yake pamoja na kuendelea kuimarisha Ofisi zilizopo. Aidha, katika kipindi hiki Ofisi imeendelea na mchakato wa mapitio ya Muundo wake wa kiutumishi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kazi ambayo bado inaendelea.

(iv) Mafunzo kwa Watumishi: Tangu kuanzishwa kwake, Ofisi imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwemo mafunzo ya kiubobevu katika maeneo maalum. Watumishi wameweza kushiriki na kufadhiliwa kwenye mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwenye Vyuo mbalimbali nchini Tanzania, Kenya, Afrika ya Kusini, Austria, na Uingereza. Halikadhalika, Ofisi imetoa Mafunzo kwa Viongozi (Menejimenti) ili kuweza kuwakumbusha misingi ya uongozi na kwa Watumishi wapya wanaoajiriwa kwa lengo la kuwaandaa kuwa Watumishi wanaofuata misingi na maaadili ya Utumishi wa umma. Mikakati iliyopo ni pamoja na kuhakikisha Ofisi inapata ongezeko la bajeti ya ya mafunzo, jambo ambalo tumekwishaanza kulifanyia kazi kwa mwaka ujao wa fedha na kuhakikisha kuwa watumishi walioanza masomo ya muda mrefu katika mwaka huu wa fedha wanaendelea kufadhiliwa ili wakamilishe mafunzo yao, kutoa ufadhili kwa watumishi wapya kwenye mafunzo ya muda mfupi na mrefu ikiwemo fursa za nafasi za kujishikiza katika Taasisi bobevu zinazokubalika na Serikali.

(v) Ujenzi wa Ofisi: Katika kuelekeza maelekezo ya Serikali ya kuhamishia shughuli zake Makao Makuu Dodoma, Ofisi imeweza kuanzisha ujenzi wa Jengo la ghorofa tano la Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma. Jengo hilo lina ukubwa wa mita za mraba 17,342 na linatarajia kugharimu kiasi cha Shilingi 26,740,706,111.79 ambacho kinajumuisha gharama za mkandarasi kiasi cha Shilingi 26,242,926,061.79 na gharama za Mshauri elekezi kiasi cha Shilingi 497,780,050.00. Ujenzi huo unatarajiwa kuwa wa kipindi cha miezi 18. Mkakati uliopo sasa na katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha ni kuhakikisha kuwa ujenzi wa jengo unatengewa fedha na unaendelea kukamilishwa katika muda uliopangwa mpaka kufikia asilimia 100.

(vi) Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri na Mifumo mingineyo ya utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Miaka Mitano Ofisi imeweza kusimika Mfumo wa usimamizi wa mashauri yanayofunguliwa na au dhidi ya Serikali. Mfumo huu umeweza kurahisisha usajili wa mashauri na kujua idadi yake kwa lengo la kuweka takwimu katika utaratibu unaotakiwa. Mikakati iliyopo ni pamoja na kuboresha matumizi ya mfumo huo ili uweze kutoa taarifa zinazojitosheleza pamoja na kuunganisha na Mifumo mingineyo ya wadau kama vile Mfumo wa Mahakama ya Tanzania ili uweze kutumika kwa ufanisi. Pamoja na Mfumo wa usimamizi wa Mashauri, Ofisi imeweza kusimika

Mifumo mingineyo ya kiserikali kwa mujibu wa maelekezo. Mifumo hiyo ni pamoja na ya masuala ya usimamizi wa taarifa (OSG-MIS), kifedha(MUSE), manunuzi(TANePS) utunzaji mali za Serikali(GAMIS) ajira na utumishi (HICMIS). Mifumo hii imeiwezesha Ofisi kuongeza uwazi, uwajibikaji na nidhamu katika matumizi ya rasilimali za Serikali.

(vii) Ununuzi wa vitendea kazi: Katika kipindi cha miaka mitano Ofisi imeweza kusimamia ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa shughuli zake na kuhakikisha usalama wa watumishi pamoja na nyaraka za Serikali ambazo wanalazimika kuwa nazo wakati wanaenda Mahakamani. Vifaa vinginevyo ni pamoja na kuhakikisha watumishi wanapatiwa komyuta za mezani na kompyuta mpakato kwa lengo la kuwawezesha kwenda na mahitaji ya Serikali mtandao (e-Government) na shughuli za kimahakama ambazo zinafanyika kwa mtandao. Mipango hii ni endelevu na itaendelea kutekelezwa katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha kama ilivyotengwa kwenye Bajeti.

(viii) Maslahi; Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi inaendelea na mikakati ya kuboresha maslahi ya watumishi ili kuongeza morali ya kufanya kazi, tija, uadilifu na watumishi kukaa sehemu moja.

(ix) Ushirikiano na wadau na ushiriki katika vyama vya kitaaluma ; Tumeendelea kushirikiana na wadau katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye utekelezaji wa majukumu yetu na kazi mbalimbali. Tunatambua michango ya wadau mbalimbali kama vile Wizara, Idara na Wakala za Serikali (MDAs), Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), Mashirika ya Umma, Mahakama, Bunge na Vyama vya Kitaaluma kama vile " The Public Bar Association" (PBA) na "Tanganyika Lawyers Society" (TLS). Mafanikio yaliyopatikana katika kuiwakilisha Serikali katika kesi za madai, usuluhishi au majadiliano ya nje ya Mahakama yasingewezekana bila ushirikiano kutoka kwa wadau wetu.

**Mwisho,** napenda kuushukuru uongozi wote wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimwa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru Viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuendelea kutusimamia vyema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi kwa miongozo anayotupatia katika kuhakikisha tunaongeza tija kwenye uendeshaji wa mashauri na taaluma. Aidha, tunaishukuru Idara ya Mahakama kama wadau wetu muhimu kwa ushirikiano wanaotupa kwa lengo la kuhakikisha tunashiriki na kuwajibika vyema katika masuala ya utoaji haki.

Kwa kuhitimisha ninawashukuru watumishi wote wa OWMS ambao wamehudumu kwenye Ofisi hii kwa nyakati tofauti na wamekuwa wakifanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa lengo la kuhakikisha tunaiishi Dira na Dhima yetu. Ninawiwa kusema kuwa nyuma ya mafanikio ya miaka mitano ni watumishi wa OWMS. Ninaamini kwa pamoja tutaendelea kusimamia misingi ya uwajibikaji, uadilifu na uaminifu katika kuhakikisha kuwa malengo, ndoto na Mikakati ya Serikali ya awamu ya sita yanafikiwa kikamilifu katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

Kazi iendelee!

# KUTOKA KWA WAKILI MKUU WA SERIKALI WA KWANZA



## DKT. JULIUS C. MASHAMBA

### Wakili Mkuu wa Serikali

### Aprili, 2018 - Julai, 2020

Kufuatia kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu tarehe 13 Februari 2018, mnamo tarehe 15 Aprili 2018, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliniteua mimi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Dkt. Ally Possi kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Kazi kubwa iliyokuwa mbele yetu wakati huo ilikuwa ni kuandaa muundo wa OWMS na kupata bajeti na ikama ya ofisi hii. Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu ilipaswa kuwa na majengo, majalada ya mashauri ya madai na usuluhishi yahusuyo Serikali, watumishi na vitendea kazi. Kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka Ofisi ya Wakili Mkuu ilifanikiwa kuyafanyia kazi masuala yote haya na hadi ilipofika Januari 2019, Ofisi ya Wakili Mkuu ilikuwa na ofisi zake na watumishi wa kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake.

Katika kipindi cha miaka miwili na nusu ya awali tangu kuanzishwa kwake, Ofisi ya Wakili Mkuu ilifanikiwa kuanzisha, kuratibu na kusimamia shughuli za kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi.

# KUTOKA KWA NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI WA KWANZA



## DKT. ALLY S. POSSI
### Naibu Wakili Mkuu wa Serikali
### Apr, 2018 - Sept, 2019

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetimiza miaka mitano, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018. Binafsi, nilipata wasaa wakuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali mwanzilishi, kama ilivyoelezewa na aliyekuwa Wakili Mkuu wa Serikali mwanzilishi, Dkt. Julius Clement Mashamba, ambapo tuliteuliwa kwa siku moja na aliyekuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mnamo tarehe 15 Aprili 2018.

nipende kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuimarisha na kuisongesha mbele Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mpaka kutimiza miaka mitano. Vilevile nimpongeze Wakili Mkuu wa Serikali na Menejimenti ya Ofisi kwa ujumla, kwa hatua Ofisi ilipofikia

Kwa sisi ambao tumepitia Ofisi hii, tunajivunia matunda ya matokeo haya. Mathalan, kuendesha mashauri ya usuluhishi sisi wenyewe, ni fanikio kubwa na limetimiza moja ya dhumuni la kuanzishwa kwa Ofisi hii. Nakumbuka siku ambayo Mawakili wetu walienda kushiriki kesi ya Sunlodges Ltd v. Tanzania, mnamo Juni 2019, pasipo kuwa na Wakili wa kigeni, ilikua ni  siku ya kipekee katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na ilitupa faraja mimi na Wakili Mkuu wa Serikali kuwa jahazi la Ofisi tumeanza lifikisha mahala salama, ni dhahiri jahazi limetia nanga na sasa lipo tayari kwa safari nyingine.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo (mwenye gauni nyeusi) akiwa katika picha ya pamoja na Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, tarehe 8 Machi, 2023*



*Baadhi ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, tarehe 8 Machi, 2023*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akikata utepe kuzindua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dodoma Agosti 15, 2018.*

# Tulipotoka: Uzinduzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilizinduliwa sambamba na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka mnamo tarehe 15 Agosti 2018 jijini Dodoma. Sherehe hizo zilihudhuriwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama mgeni rasmi wa shughuli hiyo. Katika Hotuba yake kabla ya kumkaribisha Mhe. Waziri Mkuu, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba John Kabudi alisema maneno haya:

*"Leo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya marekebisho hayo. Rais alianzisha Ofisi huru ya Taifa ya Mashtaka kuchukua nafasi ya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Rais alianzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai yakiwemo ya kikatiba ambayo Serikali ni mdaawa awali Mashauri haya yalikuwa yakishughulikiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali."*

Lengo kuu la kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kuimarisha uwezo

wa Serikali katika Kuratibu, Kusimamia, Kushauri na Kuendesha kwa ufanisi na ubora Mashauri yote ya Madai ikiwemo mashauri ya Haki za Binadamu, Katiba, Uchaguzi na Mashauri ya Usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali/Taasisi zake au yanayofunguliwa dhidi ya Serikali/ Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

Lengo mahususi la kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa ni kuimarisha huduma ya uwakili kwa Serikali na Taasisi zake ikiwa ni pamoja na kuzijengea taasisi za Serikali uwezo wa kitaalamu katika usimamizi na uratibu wa kesi zinazoihusu Serikali. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni moja ya Ofisi muhimu ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akiongozana na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi (Mb), wakati alipowasili kwenye eneo la uzinduzi wa Ofisi ya Mwanansheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dodoma, Agosti 15, 2018.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akitazama vitabu wakati alipotembelea maktaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka aliyoizindua jijini Dodoma, Agosti 15, 2018. Kulia ni aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Paramagamba Kabudi (Mb).*

# Dira na Dhima

## Dira

**Kuwa Ofisi Mahiri ya Umma ya kusimamia na kuendesha Mashauri ya Madai na Usuluhishi yanayohusu Serikali.**

## Dhima

**Kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na Usuluhishi kwa niaba ya Serikali kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu.**

Katika kutekeleza Dira na Dhima, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inazingatia maadili muhimu yafuatayo: Weledi, Uaminifu, Uadilifu, Kutokufungamana na upande wowote, kwa uhuru na kwa uwajibikaji.

# Malengo

Katika kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri yote ya Madai ikiwa ni pamoja mashauri ya Haki za Binadamu, Uchaguzi, Kikatiba na mashauri ya Usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali/Taasisi zake au dhidi ya Serikali/ Taasisi zake kwenye mahakama na mabaraza ya utowaji haki ndani na nje ya Nchi; kwa mfano Mahakama za Tanzania, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Mabaraza ya usuluhishi wa Migogoro ya uwekezaji na kibiashara.

(ii) Kuingilia kati na kuendesha mashauri ambayo Serikali ina maslahi au kugusa mali za Umma;

(iii) Kusimamia na kutoa miongozo kwa maafisa sheria na Mawakili wa Serikali ambao wanahusika katika uendeshaji wa mashauri ya Madai yanayoihusu Serikali;

(iv) Kutoa wito na maelekezo juu ya suala lolote kwa Afisa yeyote wa umma kwa ajili ya kuwezesha usimamizi mzuri wa Mashauri yote ya Madai;

(v) Kufanya vikao mbalimbali na wadau juu ya mashauri yasiyo na tija kwa Serikali na kuangalia ni kwa jinsi gani yanaweza kumalizika nje ya Mahakama na hivyo kuipunguzia Serikali gharama; na

(vi) Kuandaa Taarifa za nusu mwaka za Majukumu yanayotekelezwa na Ofisi na kuiwasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.








*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi walioshiriki katika uzinduzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali uliofanyika tarehe 15 Agosti, 2018 jijini Dodoma.*

# Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina viongozi wakuu wawili ambao ni, Wakili Mkuu wa Serikali ambaye ndiye Mkuu wa Taasisi na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ambaye ni Msaidizi Mkuu wa Wakili Mkuu wa Serikali na pia ni Afisa Masuuli ambaye anawajibika kusimamia majukumu ya kila siku na ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wote waliopo chini ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Ofisi hii ina Idara tano (5) zinazoongozwa na Wakurugenzi na Vitengo saba (7) vinavyoongozwa na Wakuu wa Vitengo. Kwa mukhtadha huo, Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina wajumbe 14 ambao ni Wakili Mkuu wa Serikali, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Wakuu wa Idara watano (5) na Wakuu wa Vitengo saba (7).

## Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kama Ulivyopitishwa na Mhe. Rais Tarehe 7 Julai, 2018



# MENEJIMENTI YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI



**DR. BONIPHACE N. LUHENDE**
Solicitor General



**SARAH D. MWAIPOPO**
Deputy Solicitor General



**GEORGE MANDEPO**
Director Arbitration



**MARK MULWAMBO**
Director Civil Litigation

Director CMQA



**JAMES KIBAMBA**
Director AHRM

Director Planning



**DEVOTA NGULUGULU**
Chief Accountant



**JOAN JOHN**
Chief Internal Auditor



**PRISCA J. ULOMI**
Head GCU



**EMIL EMMANUEL**
Head PMU



**KIUYE SHEMAKAME**
Ag. Head LSRU



**AZIZI MAKABURI**
Ag. Head ICTU



**DENNICE LEONARD**
Ag. Head LRU



**DEODATUS NYONI**
Asst. Director DL



**IRENE LESULIE**
Asst. Director IL



**HANGI CHANG'A**
Asst. Director CHRE



**DAVID KAKWAYA**
Ag. Asst. Director DA



**SALOME MAGESA**
Asst. Director IA



**CAMILIUS C. RUHINDA**
Ag. Asst. Director CM



**MERCY KYAMBA**
Asst. Director QA

# Hali ya Watumishi



*Aliyekuwa Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Gabriel Pascal Malata (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Morogoro Septemba, 2020.*

Wakati wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, mashauri yote ya Madai, Usuluhishi, Kikatiba na ya Haki za Binadamu yalikua yakiratibiwa, kusimamiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali chini ya Idara mbili (2) ambazo zilikua ni Idara ya Madai na Usuluhishi na Idara ya Katiba na Haki za Binadamu. Mashauri haya yalihamishiwa kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kuanzishwa kwake. Aidha, baadhi ya Watumishi waliokua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walihamishwa Ofisi hii ili kutekeleza majukumu yake. Hao walikuwa ni watumishi wa kwanza walioweza kuanzisha Ofisi hii mwaka 2018. Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yalitanguliwa na hatua mbalimbali za kuweka sawa mifumo ikiwemo kuandaa Muundo wa Utumishi, Kuandaa Mkataba wa Wateja; Kuandaa Mpango Mkakati wa Ofisi na kuanza utaratibu wa kupata watumishi zaidi.



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akiwa na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kikao kazi jijini Dar es Salaam Agosti, 2022.*

# Hali ya Miundombinu ya Uendeshaji Shughuli za Ofisi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianza kutekeleza majukumu yake katika Jengo ya Wizara ya Katiba na Sheria lililopo Mtaa wa Mkwepu, Jijini Dar es Salaam kabla ya kuhamishia shughuli zake katika Jengo la iliyokuwa Tume ya Mipango, Mtaa wa Kivukoni, Dar es Salaam. Wakati ilipoanza, Ofisi ilikuwa na jumla ya magari matatu (3) ambayo yalitolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wakati ilipoanza, Ofisi ilikuwa ikitunza majalada ya kesi kwa mfumo usio wa kielektroniki na hii ilisababisha baadhi ya majalada kupoteza mwelekeo mahakamani.

Mfumo wa usajili na uhifadhi wa mashauri pamoja na nyaraka ambao haukua wa kielektroni, kulikua hakuna kamera za usalama (CCTV), kifaa maalumu cha kutunzia funguo kwa ajili ya kufungulia milango ya Masjala ya Sheria, mfumo wa kuhifadhi taarifa za mashauri ambao unaweza kupatikana wakati wowote na popote.

# Uendeshaji na Usimamizi wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi

Kabla ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, baadhi ya mashauri ya kimataifa yaliendeshwa na Mawakili wa kujitegemea kupitia mikataba maalumu. Utaratibu huo haukuwa na matokeo mazuri kwa kuwa , uwajibikaji katika kuendesha mashauri ya Serikali ulikuwa hafifu; mara nyingi hukumu zilikuwa dhidi ya Serikali na pengine Serikali ilijikuta ikipata hasara kutokana na gharama zilizotumika.Pia kutokana na kutokuwepo na utaratibu wa uwajibaki, mashauri ya Serikali yalikaa muda mrefu Mahakamani pasipo kuwa na sababu za msingi.

Kwa wakati huo, mifumo iliyokuwepo haikuwezesha upatikanaji wa takwimu za uhakika za kesi za Serikali kwa kuwa hapakuwa na mfumo wa Kielektroni wa kuhifadhi na utoaji taarifa za mashauri.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, dhumuni kuu la kuanzishwa kwa Ofisi hii ilikuwa kuongeza ufanisi katika uendeshwaji wa Mashauri ya Madai yanayofunguliwa na au dhidi ya Serikali na kuondokana na mtazamo uliokuwa umezoeleka kwamba, Serikali haifanyi vizuri kwenye uendeshaji wa mashauri Mahakamani.




*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende (Wa nne kutoka Kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali baada ya kumaliza kuendesha Mashauri ya Serikali katika Baraza la Kimataifa la Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji,(ICSID) Washington Nchini Marekani mwezi Februari 2023*

# Uongozi na Utawala

Baada ya Tangazo la Serikali Na 50/2018, tarehe 14 Aprili, 2018, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Dkt. Julius Clement Mashamba kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Dkt. Ally Saleh Possi kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Aidha, tarehe 07 Julai, 2018, Mhe. Rais aliidhinisha Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali sambamba na Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ulianza rasmi mwezi Julai, 2018 baada ya Muundo wa Ofisi kupitishwa na Mheshimiwa Rais na kuwa ndiyo Mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

Tarehe 20 Septemba, 2019 Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko ya uongozi kwa kumteua Bw.Gabriel Pascal Malata ambae alikuwa Kamishna wa Kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kushika nafasi ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Mnamo tarehe 10 Julai, 2020 Mheshimiwa Rais alifanya tena mabadiliko ya uongozi kwa kumteua na kumpandisha cheo aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Gabriel Pascal Malata kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na kumteua Dkt. Boniphace Nalija Luhende aliyekuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kushika nafasi ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali.

Aidha, mnamo tarehe 09 Oktoba, 2022 Mheshimiwa Rais alifanya tena mabadiliko ya uongozi kwa kumteua na kumpandisha cheo aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende kuwa Wakili Mkuu wa Serikali, na kumteua Bi Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ambapo wote wawili waliapishwa rasmi na Mhe. Rais tarehe 22 Oktoba, 2022

Kwa maelezo hayo, tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mnamo mwaka 2018, imekuwa na Mawakili Wakuu wa Serikali watatu (3) na Naibu Wakili Wakuu wa Serikali wanne (4). Viongozi walioongoza Ofisi hii tangu kuanzishwa kwake ni kama ifuatavyo:-

### Jedwali na I: Mawakili Wakuu wa Serikali

| NA | MWAKA | | JINA LA WAKILI MKUU WA SERIKALI |
|---|---|---|---|
| | KUANZIA | MPAKA | |
| 1 | 14 Aprili, 2018 | 10 Julai, 2020 | Dkt. Clement Julius Mashamba |
| 2 | 10 Julai, 2020 | 4 Agosti, 2022 | Bw. Gabriel Pascal Malata |
| 3 | 09 Oktoba, 2022 | Mpaka sasa | Dkt. Boniphace Nalija Luhende |

### Jedwali Na II: Manaibu Wakili Wakuu wa Serikali

| NA | MWAKA | | JINA LA NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI |
|---|---|---|---|
| | KUANZIA | MPAKA | |
| 1 | 14 Aprili, 2018 | 20 Sept, 2019 | Dkt. Ally Saleh Possi |
| 2 | 20 Sept, 2019 | 10 Julai, 2020 | Bw. Gabriel Pascal Malata |
| 3 | 10 Julai, 2020 | 09 Oktoba, 2022 | Dkt. Boniphace Nalija Luhende |
| 4 | 09 Oktoba, 2022 | Mpaka sasa | Bi. Sarah Duncan Mwaipopo |

### Jedwali Na III: Wakurugenzi

| IDARA | MWAKA | | JINA LA MKURUGENZI |
|---|---|---|---|
| | KUANZIA | MPAKA | |
| Madai | 2018 | 2019 | Bw. Mark E. Mulwambo |
| | 2019 | 2020 | Bw. Vencent E.Tangoh |
| | 2020 | 2022 | Bw. Mussa I. Mbura |
| | 2023 | Hadi Sasa | Bw. Mark E. Mulwambo |
| Usuluhishi | 2018 | Hadi Sasa | Bw. George N. Mandepo |
| Menejimenti ya Kesi na Udhibiti Ubora | 2019 | 2021 | Bw. Everist M. Mashiba |
| | 2021 | April 2023 | Bw. Mark E. Mulwambo |
| Utawala na Rasilimali watu | 2018 | Hadi Sasa | Bw. James J.Kibamba |
| Mipango | 2019 | April 2023 | Dkt. Abdul A. Musa |

### Jedwali Na IV: Wakurugenzi wasaidizi

| IDARA | SEHEMU | MWAKA | | JINA LA MKURUGENZI MSAIDIZI |
|---|---|---|---|---|
| | | KUANZIA | MPAKA | |
| MADAI | Madai ya Kimataifa | 2020 | Hadi Sasa | Bi. Irene J. Lesulie |
| | Madai ya Ndani | 2020 | Hadi Sasa | Bw. Deodatus H. Nyoni |
| | Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi | 2019 | 2021 | Bi. Alesia A. Mbuya |
| | | 2021 | Hadi Sasa | Bw. Hangi M. Chan'ga |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| USULUHISHI | Usuluhishi wa Ndani | 2019 | 2023 | Bw. Ponziano L. Lukosi |
| | | 2023 | Hadi Sasa | Bw. David Kakwaya |
| | Usuluhishi wa Nje | 2022 | Hadi Sasa | Bi. Salome Magesa |
| MENEJIMENTI YA KESI NA UDHIBITI UBORA | Menejimenti ya Kesi | 2019 | 2022 | Bw. Abubakar A. Mrisha |
| | | 2023 | Hadi Sasa | Bw. Camilius C. Ruhinda |
| | Udhibiti Ubora | 2021 | Hadi Sasa | Bi. Mercy L. Kyamba |

### Jedwali Na V: Wakuu wa Vitengo

| KITENGO | MWAKA | | JINA LA MKUU WA KITENGO |
|---|---|---|---|
| | KUANZIA | MPAKA | |
| Uhasibu | 2018 | Hadi Sasa | Bi. Devota M. Ngulungulu |
| Ukaguzi wa Ndani | 2018 | Hadi Sasa | Bi. Joan L. John |
| Manunuzi | 2018 | Hadi Sasa | Bw. Emily E. Ntangwa |
| TEHAMA | 2018 | Hadi Sasa | Bw. Azizi Makaburi |
| Masijala ya Sheria | 2018 | 2019 | Bw. Mtani M. Songorwa |
| | 2019 | Hadi Sasa | Bw. Denice M. Leonard |
| Maktaba | 2020 | Hadi Sasa | Bw. Kiuye Shemakame |
| Mawasiliano | 2019 | 2022 | Bw. Innocent P. Mungy |
| | 2022 | Hadi Sasa | Bi. Prisca Ulomi |

### Jedwali Na VI: Mawakili Wafawidhi wa Mikoa

| NA. | JINA | MKOA/ KANDA |
|---|---|---|
| 1. | Peter Mseti | Arusha |
| 2. | Yohana Marco | Moshi |
| 3. | Rashid Mohamed | Tanga |
| 4. | Mjahid Kamugisha | Sumbawanga |
| 5. | Gerald Njoka | Kagera |
| 6. | Kitia Turoke | Mara |
| 7. | Subira Mwandambo | Mwanza |
| 8. | Solomon Lwenge | Shinyanga |
| 9. | Lameck Melumba | Tabora |
| 10. | Masunga Kamihanda | Mtwara |
| 11. | Egidy Mkolwe | Ruvuma |
| 12. | Jenipher Kaaya | Dodoma |
| 13. | Allan Shija | Kigoma |
| 14. | Rodgers Massawe | Mbeya |
| 15. | Exavery Ndalawa | Morogoro |
| 16. | Ansila Makyao | Iringa |




# TULIPO SASA: UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI NA MAFANIKIO KUANZIA JULAI 2018- MACHI 2023

Katika kutekeleza Dira na Dhima ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, katika kipindi kinachoanzia 2018/2019 hadi 2022/2023 Ofisi ilikuwa na malengo na vipaumbele ambavyo vilitumika katika kuandaa bajeti kwa kipindi husika. Sura hii inaeleza malengo na vipaumbele, mafanikio katika utekelezaji pamoja na changamoto.

Malengo na maeneo ya vipaumbele vya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kipindi chote toka kuanzishwa kwake yamekuwa yakiandaliwa kwa kuzingatia Mipango ya Taifa ya Maendeleo, Dira ya Taifa ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Tawala kwa kipindi husika.

## MALENGO MAHSUSI

Malengo Mahsusi ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kama ifuatavyo:-

i. Kuiwakilisha kwa Ufanisi na Ubora Serikali na taasisi zake katika mashauri yote ya Madai na Usuluhishi ikiwemo Madai ya Kikatiba, Haki za Binadamu na Utawala Bora;

ii. Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora;

iii. Kuboresha masuala ya kiutawala, usimamizi wa rasilimali fedha na uwezo wa Taasisi kuimarishwa pamoja na kuboresha ushiriki wa wadau na uimarishwaji wa

taratibu pamoja na miundombinu ya TEHAMA.

## MALENGO MTAMBUKA

i. Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI, magonjwa yasiyoambukizwa pamoja na kuboresha huduma kwa waathirika:

Katika lengo hili Ofisi ina mkakati wa kupunguza maambukizi mapya ya VVU, Ukimwi na magonjwa yasiyoambukizwa na kuboresha huduma kwa waathirika kwa kutoa huduma bora na msaada wa chakula kwa waathirika (lishe), kuongeza kampeni katika kutoa Taarifa, elimu, na upimaji wa VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na kutoa uelewa juu ya kupunguza magojwa yasiyoambukizwa.

ii. Kuimarisha Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa na kupunguza matukio yatokanayo na rushwa

Katika lengo hili Ofisi inasimamia mkakati wa Taifa wa mapambano dhidi ya rushwa kwa kwa kutoa elimu kwa watumishi juu ya madhara ya rushwa na athari zake kwa jamii kwa lengo la kupunguza na kuondoa matukio yatokanayo na rushwa .

## MAENEO YA VIPAUMBELE

Katika kuhakikisha kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inafikia malengo, Ofisi imeainisha maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:

i. Kuendelelea kuratibu, kusimamia na kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi;

ii. Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Dodoma;

iii. Kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwemo mafunzo ya kiubobevu katika maeneo maalum pamoja na kuwapeleka katika ofisi nyingine kwa ajili ya uzoefu ndani na nje ya nchi;

iv. Kuimarisha ofisi za Mikoa ili kupeleka huduma karibu na taasisi na ofisi za Serikali zilizoko katika mikoa husika pamoja na wananchi, ambapo kwa sasa Ofisi ina jumla ya ofisi katika mikoa 17 ambayo ina Mahakama Kuu. Aidha Ofisi ina mpango wa kuendelea kufungua ofisi kwa kila mkoa ulio na Mahakama Kuu;

v. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa Usimamizi wa Mashauri ili kuhakikisha kuwa mifumo inasomana na mifumo ya ofisi nyingine ambazo zinashirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu kama vile Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama, Ofisi ya Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

vi. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi pamoja na maendeleo ya rasilimali watu.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake tangu mwaka 2018 ilipoanzishwa imeweza kutekeleza shughuli nyingi za kiofisi na kiutendaji ikiwemo, Kusimamia Mashauri ya Madai na Usuluhishi, kuongeza watumishi pamoja na kuboresha miundombinu ya kiutendaji katika ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

**A. Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika mashauri yote ya Madai na Usuluhishi ndani na nje ya nchi.**

i. Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuwa na kituo jumuishi cha kusimamia uendeshwaji wa Mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayohusu serikali na taasii zake. Hii imesaidia kuratibu mashauri kwa uangalizi wa karibu na kuipunguzia Serikali gharama kwa kusitisha utaratibu wa zamani wa kutumia mawakili wa kujitegemea na badala yake kutumia utaratibu mpya wa kutumia Mawakili wa Serikali kuendesha mashauri ya Serikali.

ii. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeanzisha Ofisi za Mikoa kumi na sita (16) nchini na hivyo kuweza kuratibu uendeshaji wa mashauri katika Mkoa kumi na sita (16) zenye Masijala ya Mahakama Kuu ikiwemo Morogoro, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Arusha, Tanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Kagera, Tabora, Musoma, Kigoma, Songea, Mtwara, Sumbawanga na Iringa. Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatarajia kufungua ofisi mkoani Manyara hivi karibuni.

iii. Kuongeza ufanisi katika uendeshwaji wa Mashauri yanayoihusu Serikali kwa kuepusha mashauri mengi ya Serikali kusikilizwa upande mmoja.

iv. Kufanya uchambuzi wa kina wa notisi za madai dhidi ya Serikali kwa mashauri yanayokusudiwa kufunguliwa Mahakama na Mabaraza ya Usuluhishi. Utaratibu huo umekuwa na tija kubwa kwa Serikali katika kupunguza gharama za Mashauri; kuleta maelewano mazuri pamoja baina ya Serikali na watoa huduma na wawekezaji. Pia imewesha wawekezaji kuendelea na utekelezaji wa miradi na hivyo kuiwezesha nchi kunufaika.

v. Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika Mashauri ya Madai na Usuluhishi ambapo Serikali imeshinda mashauri ya Madai na Usuluhishi yenye thamani ya zaidi ya Shilingi za Tanzania Trilioni saba (7) fedha ambazo endapo ofisi isingeshughulikia Mashauri hayo, Serikali ingelazimika kulipa fedha hizo kwa Wadai.

vi. Kuwezesha Serikali kuwa na uwakilishi mzuri kwenye Mashauri kupitia uwakilishi unaofanywa katika Mahakama na Mabaraza ya Usuluhishi. Uwakilishi huo umeiwezesha Serikali kushinda kesi mbalimbali na kurejesha mali mbalimbali zilizohusisha ardhi, mashamba, nyumba za Serikali na kadhalika.

vii. Kuchangia katika maboresho ya sheria mbalimbali ambapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kutoa maoni ya maboresho ya sheria hususan zile zinazohusu uendeshaji wa mashauri ya Serikali.

viii. Kupatanisha Taasisi za Serikali zilizofunguliana mashauri Mahakamani au kwenye mabaraza Usuluhishi ambapo Mashauri yamekuwa yakiondolewa Mahakamani au kwenye mabaraza na kisha Taasisi kujadiliana namna bora ya kutatua migororo iliyopo kwa njia mbadala hivyo kuimairisha ushirikiano baina ya Taasisi za Serikali.

ix. Kuhamasisha Taasisi za Serikali na Mashirika ya umma kuwasilisha Mashauri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuratibiwa na kusimamiwa na hivyo kuipunguzia Serikali gharama za ada ya uwakilishi Mahakamani kupitia Mawakili wa kujitegemea.

x. Katika kusimamia viwango vya utendaji kazi wa Mawakili, Ofisi ya Wakili Mkuu

wa Serikali imefanikisha uandaaji wa nyaraka za Kuratibu Viwango vya ubora, Miongozo ya Mashauri ya Madai na Usuluhishi pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Wateja. Nyaraka hizo zimefanikisha kwa kiwango kikubwa kuboresha utendaji kazi wa Mawakili ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo ya namna ya uandishi wa nyaraka za kisheria, mavazi ya mahakamani, maandalizi ya mashauri Mahakamani, kusiliza na kuhudumia wateja wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

xi. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuanzisha Mfumo wa Mashauri wa Kielektroni ambao unahusika na usajili wa Mashauri, upangagji wa Mashauri kwa mawakili, uingizaji wa taarifa mbalimbali za Mashauri pamoja na upatikanaji ya taarifa muhimu zinazohusu Mashauri kwa njia ya mtandao wakati wote na mahali pote duniani. Mfumo huu umesaidia pia kupunguza muda wa uandaaji wa ripoti mbalimbali za Mashauri pamoja na kujua idadi za Mashauri kwa kila wakili na hivyo kusaidia katika ugawaji wa majukumu.

xii. Uratibu na ushiriki katika maadhimisho ya wiki ya sheria toka kuanzishwa kwa ofisi ambayo yamesaidia sana katika kuitangaza ofisi na kazi zake. Maadhimisho haya yamechangia katika kujenga mahusiano mazuri na Taasisi nyingine ambao ni wadau wa Mahakama hivyo kuwa sehemu ya utendaji haki na kuchangia katika maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

xiii. Uandaaji na utoaji Hati Idhini kwa Mawakili wa Serikali nchini pamoja na kuwafanyia ukaguzi Mawakili wanaopewa idhini hizo wakati wa uendeshaji wa mashauri Mahakamani. Hati hizi zimesaidia kuongeza Usimamizi wa Mashauri pamoja na uwajibikaji katika kuendesha Mashauri katika taasisi husika.

xiv. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuandaa taarifa ya kila nusu mwaka tangu kuanzishwa na hivyo kufanikisha matakwa ya kisheria pamoja na upatikanaji wa taarifa za shughuli za ofisi za kila miezi sita kwa wadau hivyo kuendelea kuonesha umuhimu wa ofisi yetu katika Taifa letu.

xv. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuboresha Mifumo ya Usalama wa Nyaraka kwa kuboresha miundombinu ya ofisi kama Kufunga kamera za Usalama (CCTV), kutenga maeneo ya uhifadhi wa nyaraka ili kutoruhusu wasihusika kuingia ndani pamoja na kufunga kifaa maalumu cha kutunza funguo kwa ajili ya kufungulia Milango ya Masjala ya Sheria

xvi. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweka Mfumo unaoweza kutambua Taasisi za Serikali zenye Mashauri na migogoro mingi inayoweza pelekea Serikali kuingia hasara na kupoteza fedha nyingi kwa njia ya kupitia notisi za nia za kuishtaki Serikali kufanya vikao vya na kuweza kutatua baadhi ya migogoro nje ya Mahakama.

## B. Mawasiliano Serikalini, TEHAMA, Maktaba pamoja na Utafiti.

i. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kuelimisha na kuhabarisha umma kwa kutoa taarifa mbalimbali za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa wadau na wananchi kwa ujumla ikiwemo uchapishaji wa nakala 2,250 za Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali; makala 120; machapisho na vipeperushi 750; vipindi maalum 3 vya

runinga; mabango ya mtandaoni 25;

ii. Uanzishwaji na uwepo wa tovuti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo inatoa taarifa mbalimbali kwa jamii pamoja na kurahisisha mawasiliano kupitia mfumo wa barua pepe za serikali.

iii. Uwepo wa mfumo wa masijala mtandao, mfumo ambao unarahisha mzunguko wa majalada na kuwawezesha watumishi kuokoa muda na fedha katika kushughulikia masuala mbalimbaliya kiofisi sambamba na kufuatilia mienendo ya majalada na barua, katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa njia ya mtandao.

iv. Uboreshwaji wa mtandao kiambo (LAN) ambao unarahisisha kupata huduma ya mawasiliano ya intanet kwa watumishi.

v. Uwepo wa kompyuta za mezani, kompyuta mpakato na printa zinazowawezesha watumishi kufanya kazi na kutoa ripoti kwa urahisi.

vi. Tumeweza kujiunga katika Mfumo wa mawasiliano Serikalini ambao unatoa huduma ya mtandao na mifumo ya kiserikali kwa urahisi.

vii. Kuunda mfumo wa kuhifadhi na kutoa taarifa za mashauri yanayoendeshwa na Ofisi yetu (Case Inventory Management System).

viii. Uwepo wa Sera ya TEHAMA, na kwa sasa ofisi inaandaa Miongozo itakayosaidia usimamizi na endeshaji salama wa masuala yote ya TEHAMA katika Ofisi yetu.

ix. Kuandaa rejesta ya marejeo ya sheria kwa kujumuisha mashauri yaliyoamuliwa na Mahakama ya Rufani. Marejeo hayo yamewekwa katika mtandao wa Maktaba www.elibrary@osg.go.tz ambao kwa kiasi kikubwa unawasaidia sana Mawakili kufanya marejeo wakati wa maandalizi ya kuendesha mashauri Mahakamani.

x. Kukusanya na kuandaa juzuu za Sheria mbalimbali zinazohusu uendeshaji wa mashauri ya Madai na Usuluhishi na nyingine ambazo zinahusisha masuala ya msingi kwenye kuwezesha Mawakili kuendesha Mashauri za Serikali;

xi. Kusambaza hukumu za Mashauri mbalimbali ya Tanzania ambayo hayajaripotiwa na kuwasilishwa kwa Mawakili wa Serikali kwa njia ya barua pepe kwa mfumo wa kielektroni, pamoja na nakala ngumu;

xii. Ofisi imewezesha upatikanaji wa vitabu zaidi ya 1,300 vya taaluma mbalimbali;

xiii. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikai imeanzisha maktaba ya Kielektroniki (D-SPACE Repository) ambapo Machapisho na nyenzo za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zinaweza kupatikana kupitia www.elibrary@osg.go.tz.

## C. Utawala na Rasilimali Watu

Katika kipindi cha miaka mitano tangu kuanzishwa, ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ofisi imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

i. Kufungua Ofisi za Mikoa

Ofisi imefungua Ofisi katika Mikoa kumi na saba (17) ambayo kwa sasa ina Masijala za Mahakama Kuu na kuendelea kuboresha mazingira ya ofisi hizo. Ni matarajio yetu kuwa tutaendelea kufungua ofisi kwenye kila mkoa ambao Mahakama itafungua masijala za Mahakama kuu.

ii. Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi

Katika kutekeleza mpango wa pamoja wa ujenzi wa vituo jumuishi vya Taasisi za Kisheria, Mnamo mwezi Novemba, 2022; Ofisi ilishiriki uzinduzi wa ujenzi wa jengo jumuishi la taasisi za kisheria

jijini Mwanza. Lengo likiwa ni kusogeza huduma za kisheria na utoaji wa haki karibu na wananchi.

iii. Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu Dodoma

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tayari imeanza Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu yake katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Jengo hilo ni la ghorofa tano (5). Jengo hilo linajengwa kwenye kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 17,342 Muda wa ujenzi wa mradi huu ni miezi kumi na nane (18).

iv. Ununuzi wa Magari

Katika kipindi cha miaka mitano, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kununua magari mapya 31 na kufanya Ofisi kuwa na jumla ya magari 35. Kuongezeka kwa idadi ya magari kumesaidia kuwa na usafiri wa uhakika ambao unarahisisha utekelezaji wa majukumu hayo na pia kuwahakikishia usalama watumishi pamoja na nyaraka za Serikali ambazo wanalazimika kuwa nazo wakati wanaenda Mahakamani.

v. Kushiriki Mikutano:

Ofisi iliweza kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali ulioandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuzindua Chama cha Mawakili wa Serikali (Public Bar Association)

vi. Mafunzo kwa Watumishi:

Katika kipindi cha miaka minne (4) tangu kuanzishwa kwake, Ofisi imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwemo mafunzo ya kiubobevu katika maeneo maalum,

a. Katika kipindi husika, jumla ya watumishi 27 wamepatiwa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu. na watumishi 26 walipatiwa ufadhili wa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

b. Ofisi imeweka utaratibu wa kila mwaka wa kuwa na mafunzo yanayohusu masuala ya Mashauri za madai na usuluhishi kwa Mawakili wote wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wizara na Idara za Serikali ikiwemo TAMISEMI.

c. Mafunzo kwa Menejimenti ili kuweza kuwakumbusha mambo ambayo wanapaswa kuyafanya na kuyaishi kama viongozi;


**D. Mipango, Fedha, Manunuzi na Ukaguzi**

i. Ofisi imeweza kufikia malengo yake kwa kufanya kutathmini na kuzingatia ushauri unaotokana na hoja za ukaguzi na hivyo kuweza kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na utawala bora.

ii. Ofisi imeweza kusimamia mifumo ya udhibiti pamoja na ufungaji wa hesabu na kupelekekea kupata hadi safi katika kipindi chote.

iii. Ofisi imeweza kutekeleza shughuli za manunuzi kwa kwa pitia mfumo wa TANePS.

# HABARI NA MATUKIO KATIKA PICHA




*Muonekano wa dashibodi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri*




*Mfumo wa Maktaba Mtando wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende, akiwaongoza watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika mafunzo ya elimu ya afya, upimaji wa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.*



*Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria akiweka jiwe la msingi la jengo Jumuishi la Taasisi za Sheria lililopo eneo la Buswelu Wilayani Ilemela Mkoani Mwanza Novemba, 2022. Kutoka kulia ni Dkt. Khatibu Kazungu, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Boniphace Luhende Wakili Mkuu wa Serikali na Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*



*Mawakili wa Serikali wakiwa katika mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyofanyika jijini Arusha Juni, 2022.*



*Wakili Mkuu wa Serikali akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria Februari, 2022 Jijini Dodoma.*



*Afisa Tawala Mwandamizi Geoffrey Annaniah (kushoto) akimkabidhi gari Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kigoma Allan Shija*

# CHANGAMOTO

**Zipo changamoto mbalimbali ambazo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekutana nazo katika kipindi cha miaka mitano. Baadhi ya changamoto hizo ni:**

(a) Ufinyu wa Bajeti ambako kumechangia Ofisi kushindwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Ufinyu huo wa bajeti kwa kiasi kikubwa umeathiri maeneo yafuatayo;

i. Upungufu wa fedha za maandalizi ya mashauri, uendeshaji wa mashauri ndani na nje ya nchi ikiwemo majadiliano ya kumaliza migogoro na mashauri nje ya mahakama.

ii. Mafunzo ya ndani na nje ya nchi ambapo watumishi 27 wamepatiwa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kati ya watumishi 52 walioomba kupatiwa mafunzo hayo na watumishi 26 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kati ya watumishi 181 wanaohitajika kupatiwa mafunzo hayo.

iii. Upungufu wa vyombo vya usafiri kwa ajili kuwezesha Mawakili kwenda Mahakamani na usalama wa watumishi wanapotekeleza majukumu ya ofisi;

iv. Kukosekana kwa bajeti ya maendeleo ili kuwezesha ujenzi wa majengo ya vituo jumuishi katika mikoa ya Tabora na Dodoma.

(b) Upungufu wa Watumishi kulingana na kuongezeka kwa majukumu;

(c) Upungufu wa watumishi wenye weledi wa kitaaluma.

(d) Kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya wadau ambao wana mashauri chini ya Ofisi;

(e) Baadhi ya Watendaji wa Serikali kufanya maamuzi pasipo kuzingatia sheria na taratibu.

# MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO PAMOJA NA MATARAJIO




*Mwonekano wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linaloendelea kujengwa katika mji wa Serikali mtumba jijini Dodoma.*

Matarajio katika utekelezaji wa Majukumu, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatarajia kuendelea kuboresha utendaji pamoja na Usimamizi wa Mashauri kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea kutekeleza majukumu mengine kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sheria ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Office of the Attorney General Discharge of Duties Act, CAP 268 R.E 2019), Kanuni za Kurekebisha uundwaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tangazo la Serikali Namba 49/2018 (Office of the Attorney-General (Re-structure) Order, 2018) Kanuni za kuanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Tangazo la Serikali Namba 50/2018 (Office of the Solicitor-General Establishment Order, 2018), Sheria ya Mwenendo wa Uendeshaji wa Mashauri ya Serikali (Government Proceedings Act, R.E 2019) kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2019 na sheria nyingine.

ii. Kuendelea kulinda na kutetea maslahi ya Serikali katika mashauri yote yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali;

iii. Kuendelea kujengeana uwezo Mawakili kwa kufanya na kuratibu mafunzo ya mara kwa mara kwa kuwapa ujuzi katika sekta mbalimbali kulingana na mabadiliko na maendeleo ya nchi, kama vile uwekezaji, uchumi wa bluu, majadiliano na menejiment ya mikataba (contract management & negotiations), nishati

mbadala na nishati jadidifu, mali asili na utalii.

iv. Kuendelea kuongeza mashirikiano na wadau wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambao ofisi inaendesha mashauri kwa lengo la kutatua changamoto zinazojitokeza katika uendeshaji wa mashauri na kusaidia Serikali kuondokana na migogoro isiyo na msingi.

v. Ofisi inatarajia kuendelea kuomba vibali vya ajira ili kuongeza idadi ya watumishi katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye ofisi zote nchini.

vi. Kusimika mfumo wa usimamizi wa shughuli na rasiliamli za Ofisi, mfumo ambao utasimamia shughuli zote za Utawala, Uhasibu, Mipango na Manunuzi na kufanya Ofisi hizi kutekeleza shughuli zake kwa weledi.

vii. Kuboresha mifumo mbalimbali ya kimtandao ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi na uhabarishaji.

viii. Kuendelea kufanya majadiliano na Serikali ili kuomba kuongezewa wigo wa bajeti (ceiling) ya kawaida na ya maendeleo ili kuweza kutoa huduma stahiki na kuboresha mazingira ya kazi.

ix. Kuendelea kuwajengea uwezo Mawakili kwa kuwapatia mafunzo ya uendeshaji mashauri kwenye maeneo ya kimkakati kama vile uwekezaji, madini, mafuta na gesi na kuhakikisha kuwa tunawatumia Mawakili wa ndani kuendesha Mashauri yote ya ndani na nje ya nchi pale ambapo sheria zinaruhusu kufanya hivyo.



*Baadhi ya Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakikagua mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali unaoendelea katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma, Mei, 2023*







*Sehemu ya Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki maadhimisho ya Mei Mosi 2023 wakiwa katika picha ya pamoja uwanja wa Uhuru Dar es Salaam*



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakiwa viwanja vya Chinangali kwa ajili ya kushiriki kilele cha Maadhimisho ya wiki ya Sheria jijini Dodoma, February 2023.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (aliesimama katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maadhimisho ya wiki ya Sheria Februari, 2023.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO
## OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 321<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Chumba Na. 13 na 15<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |